# TARGETER WINGS
## KENYA JUNIOR SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT
## GREDI YA TISA - 2026

Wings 001

## KISWAHILI: LUGHA

Muda: Saa 1 dakika 40

| | |
|---|---|
| Jina la Mtahiniwa ____________ | Nambari ya Mtahiniwa ____________ |
| Jina ya Shule yako ____________ | Nambari ya Shule ____________ |
| Sahihi ya mtahiniwa ____________ | Tarehe ____________ |

| MTAHINI PEKEE | | | |
|---|---|---|---|
| Swali | Upeo wa alama | Alama ya mwanafunzi | Kiwango cha utendaji |
| 1-50 | Alama 50 | | |
| Jumla | 50 | | |

**KJSEA**
**902/1**
**KISWAHILI LUGHA**
**Karatasi ya 1**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

1. Umepewa **kijitabu** hiki na **karatasi ya majibu**. Kijitabu hiki kina maswali **50**.
2. Jibu maswali **yote** kwenye **karatasi ya majibu** uliyopewa kujibia maswali na wala **sio** katika kijitabu hiki.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida, aina ya HB.
4. Hakikisha kuwa karatasi ya majibu uliyopewa ina:
   **NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
   **JINA LA SOMO**
5. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
6. Kwa kila swali, **1 – 50** umepewa majibu manne, **A, B, C, D.** Chagua **jibu sahihi.**
7. Kwenye karatasi ya majibu, onyesha jibu sahihi kwa **kuchora kistari** katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa jibu sahihi.

**Mfano:**
**Katika kijitabu cha maswali:**

25. **Kamilisha sentensi:**
Kisawe cha bwanyenye ni ____________

A. maskini
B. kipusa
C. fukara
D. tajiri

**Jibu sahihi ni 'D'.**
**Katika karatasi ya majibu,** palipo na visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **25,** chora kistari ndani ya kisanduku chenye herufi **D.**

**25.** **[A]** **[B]** **[C]** **[D]**

8. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
9. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu, kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**
**Hakikisha kuwa kurasa zote zipo na maswali yapo ipasavyo.**



CamScanner

## SEHEMU A

## I. UFAHAMU WA KUSOMA

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 6:***

Lengo langu nilipojiunga na shule ya upili ya Pepea ilikuwa ni kusoma kwa bidii hadi kileleni. Nilichochewa na ari ya kutaka kupata alama za juu katika mitihani yote. Nikajifunga kibwebwe na kutia bidii za mchwa ili nitimize ndoto yangu. Nilielewa vyema kuwa mtaka cha mvunguni sharti ainame.

Maisha ya shuleni yalikuwa ya upweke nilipojiunga na gredi ya kumi. Sikuwa na marafiki wa **kupiga soga** nao na kujuliana hali za makwetu. Kweli upweke ni uvundo na upweke uliponizidia, niliona haja ya kufanya urafiki na msichana mmoja tuliyesoma naye kwa jina Karina.

Mwanzoni, usuhuba wetu ulikuwa wa kufana. Tulifaana kwa dhiki na furaha. Tulishinda na kufanya shughuli zetu pamoja sawa na kusaidiana masomoni. kusaidiana huku kulituwezesha kupiga hatua kubwa na kuwapiku wenzetu. Ufanisi wetu masomoni hata hivyo, haukuwapendeza wengi. Nakumbuka wakati mmoja nikiwa ninapita karibu na kijia kilichoelekea bwenini wakati wa usiku, nilisikia minong'ono ya wanafunzi.

Sikuamini nilichosikia, walikiri kuwa nilikuwa mwizi. Eti nilitumia uchawi kupita mtihani, siku chache baada ya mmoja wetu kupoteza pesa zake shilingi mia tatu sanduku langu lilikuwa la kwanza kusakwa. Vitu vilipopotea shuleni tangu hapo, nilikuwa mshukiwa wa kwanza. Walimu wakapoteza imani nami na kunichukia. nikawa kinyago cha kuchekwa.

Nilipokosa stahamala, niliamua kuchunguza chanzo cha tuhuma zilizoninyeshea. Sikuamini kuwa yule msiri wangu niliyemwamini kwa moyo wangu wote ndiye aliyenila kivuli. Karina, mwandani wangu, msiri wangu aliwezaje kunisaliti namna hiyo? Karina ndiye aliyekuwa akieneza uongo wote huo. Nilipogundua alinijia na kuniangukia kwa kutaka radhi zangu lakini nilijua fika kuwa urafiki wetu haungezoleka. Hapo ndipo nilipobaini kuwa kikulacho ki nguoni mwako!

**1.** Kulingana na aya ya kwanza msimulizi
- A. alikuwa na nia ya kuelekea kileleni
- B. alipenda masomo
- C. alipenda kuota ndoto za kushangaza
- D. alikuwa mchochezi

**2.** Urafiki kati ya Karina na msimulizi ulianza
- A. punde tu alipojiunga na shule ya Pepea
- B. msimulizi alipokuwa mgeni shuleni
- C. aliposhindwa kustahimili kuwa peke yake
- D. mitihani ilipokaribia

**3.** Chagua jibu linaloonyesha kuwa alikuwa mwenye bidii
- A. kila mara aliwapiku wenzake kwenye mtihani
- B. alitumia nguvu za uchawi kufaulu
- C. alikuwa akisomea shule ya bweni
- D. kila walipofanya mitihani alimshinda Karina

**4.** Maana ya kauli kupiga soga kwa mujibu wa kifungu ni;
- A. kuwasaidia wengine
- B. kusoma kwa bidii
- C. kupiga kelele darasani
- D. kuzungumza ili kupitisha wakati

**5.** Mambo yafuatayo yalimfanyikia msimulizi isipokuwa
- A. kusoma kwa bidii
- B. kupewa uchawi na Karina
- C. kuchukiwa shuleni na kila mtu
- D. kuchukiwa na walimu wake

**6.** Chagua methali mwafaka inayoafiki kifungu hiki.
- A. Ndugu ni kufaana si kufanana
- B. Kikulacho ki nguoni mwako
- C. Mui huwa mwema
- D. Asiyekujua hakuthamini



CamScanner

## UFAHAMU

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 7 hadi 12:***

Nyani aliwaza usiku kucha. Hakupata hata lepe la usingizi. Starehe ya usingizi ingetoka wapi ikiwa vurumai na mahangaiko yalimwacha fukara? Maskini asiye na mbele wala nyuma ?
Aliwatupia jicho wanawe waliolala karibu naye. Hata hawakuwa na habari kuhusu yaliyokumba eneo zima la Kaukeni. Vilevile hawakuwa na habari kuhusu baba yao. Hicho kilikuwa kitendawili ambacho Nyani alihitaji kuwategulia wanawe. Lakini hata angekitegua salama ingetoka wapi?

Mume huyo ambaye ni mfano tu wa mume kamwachia mateso yasiyopimika, kamwachia umaskini usio na mfano na mashaka yasiyomwisha. Lau angalijua aliko, angaliomba dua atokomee kabisa katika uso wa dunia. Wazo hili lilipomjia alishtuka na kuwaza. Kwa nini? Hajawahi hata siku moja kumwazia yeyote maovu, sembuse mumewe. Mume aliyekuwa mwandani wake wa karibu, aliyemfariji na kumkinga dhidi ya manyanyaso ya Sungura, Mbweha na wanyama wengine pale kazini. Akamhifadhi na kumtunza katika mawazo yake, alilikemea wazo hilo. Lakini kila alipolikemea ndivyo lilivyorudi kwa nguvu na kuiponza nafsi yake. Wazo sasa lilimtaka asimtie mumewe akilini tena. Amsahau kama vile mtoto anavyolisahau titi la mama yake. Alipofika hatua hii, alijikuta akitetemeka kama aliyemwagiwa maji ya barafu. Woga ukamvaa.

Hatimaye aliomba Mungu amwepushie mabaya kokote alikokuwa mumewe. Alimwomba asiruhusu mauti au hatari yoyote kumkaribia mumewe. **Bado alimhitaji hata kama alimtupa kama tambara bovu.** Wanawe pia walimhitaji. Alipowatazama wanawe, machozi yalianza kumtiririka njia mbili akiwaza jinsi atakavyowalisha siku hiyo.

**7.** Kwa mujibu wa **aya ya kwanza,** mawazo ya Nyani yalitokana na:

A. ukosefu wa usingizi

B. umaskini uliomkabili.

C. wanawe waliolala

D. matatizo yaliyomkabili

**8.** Chagua jawabu lililo **sahihi**

A. Familia ya Nyani ilikuwa fukara

B. Watoto wa Nyani hawakumjua baba yao

C. Wanawe Nyani walimtegemea mama yao.

D. Mkewe Nyani alipenda kuwategea wanawe vitendawili.

**9.** Nyani alikabiliwa na shida zifuatazo **isipokuwa**

A. Kuwalea wanawe bila usaidizi wa mume

B. Upweke wa kuishi bila mume

C. Kunyanyaswa na wanyama wenzake

D. Kukosa namna ya kujipatia riziki

**10.** Kauli, **"Bado alimhitaji hata kama alimtupa kama tambara bovu."**
Imetumia mbinu gani ya lugha ?

A Tashbihi | B. Nahau

C. Chuku | D. Tashhisi

**11.** Ni ipi si sifa ya mkewe Nyani kwa mujibu wa kifungu hiki?

A. Mvumilivu | B. Msamehevu

C. Mwenye roho mbaya | D. Mlezi mwema.

**12.** Chagua jawabu lisilo sahihi kwa mujibu wa kifungu hiki.

A. Nyani hakutaka mume wake apatwe na lolote baya.

B. Nyani hakumhitaji tena mume wake maishani

C. Wanawe Nyani hawakuwa na chakula nyumbani kwao.

D. Nyani alimtakia mema mume wake kokote alikokuwa.

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali kutoka 13-17**

Usalama barabarani ni jambo la kutiliwa maanani na kila mtumizi wa barabara. Madereva wanastahili **kukaa ange** barabarani ili wasisababishe ajali. Madereva wote wanapaswa kujali maisha ya abiria na hata wao binafsi. Magari yanafaa kutiwa vidhibiti mwendo ili yasisababishe ajali. Wanaovunja sheria wakabiliwe na mkono mrefu wa serikali hususan wanapovunja sheria za barabarani.

Waendeshaji bodaboda wanapaswa kuwa waangalifu sana. Aghalabu ajali nyingi huhusisha pikipiki. Waendeshaji hao mara nyingi huendesha pikipiki kwa kasi na kuwagonga wapita njia ama kutatiza waendeshaji magari na hatma yake huwa ni ajali. Kuna wale ambao pia huendesha pikipiki upande usiofaa wa barabara na kusababisha ajali. Idadi kubwa ya waendeshaji Pikipiki hupuuza sheria za barabarani, baadhi hawavai helmeti, hutumia mihadarati na kubeba abiria zaidi ya mmoja.

Kila mpitanjia anapaswa pia kuwajibika na kuwajibikia usalama wake na wa wenzake. Watumie sehemu iliyotengwa kwa ajili yao wanapovuka barabara. Watumie kivuko milia ipasavyo, wahakikishe pande zote za barabara hazina magari, baiskeli au pikipiki wanapovuka.

Ni jukumu la kila mtu kujali maisha yake na ya wenzake anapotumia barabara. Kumbuka, maisha ni mshumaa uso mkesha.

---

**13.** Kifungu kimebainisha kuwa kila dereva;

A. awe na leseni ya kuendesha gari au pikipiki.

B. aepuke ajali kwa kila namna

C. atumie barabara apendavyo.

D. aendeshe gari lake kwa kasi.

**14.** Je, unadhani ni kwa nini magari yote yanapaswa kuwa na vidhibiti mwendo?

A. Ili kuzidisha kasi ya magari

B. Ili kuepuka ajali barabarani

C. Ili Kumudu kasi ya gari.

D. Kumtahadharisha dereva.

**15.** Sheria za barabarani hupuuzwa kwa njia zifuatazo isipokuwa:

A. Kuendesha pikipiki au gari katika upande usiofaa wa barabara

B. Kufunga mkanda wa usalama

C. Kutovaa helmeti

D. Kuendesha kwa kasi

**16. Kukaa ange inamaanisha nini?**

A. Kutolala barabarani

B. Kuwa tayari kufanya jambo

C. Kukaa imara barabarani.

D. Kuchukua tahadhari

**17.** Methali, **'Maisha ni mshumaa uso mkesha'** hutueleza ukweli kuwa:

A. Maisha hayadumu

B. Maisha na mauti ni sawa

C. Jambo tusilofaa kufanya tuachane nalo

D. Maisha huwa na usumbufu.



CamScanner

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 18 hadi la 20**

Wanafunzi wa shule ya Tumaini huwa na ratiba ya mimea inayopandwa shuleni kila jioni. Tazama jedwali hili.

| Siku / Mimea | Jumatatu | Jumanne | Jumatano | Alhamisi | Ijumaa |
|---|---|---|---|---|---|
| Mipera | ✓ | ✓ | | ✓ | |
| Mikahawa | | | ✓ | | |
| Michai | ✓ | | | ✓ | |
| Miparachichi | ✓ | ✓ | | ✓ | ✓ |
| Mipapai | | | ✓ | | ✓ |
| Minyanya | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Mizabibu | | ✓ | | | ✓ |

**18.** Chagua jibu linaloonyesha mimea inayopandwa mara mbili pekee kwa wiki.

A. Mizabibu, mipera, michai
B. Michai, mipera, miparachichi
C. Mizabibu, mipapai, michai
D. Mipapai, michai, miparachichi

**19.** Ni Siku gani ambapo wanafunzi wa shule ya Tumaini hupanda mimea michache zaidi?

A. Jumanne
B. Jumatano
C. Alhamisi
D. Jumaa

**20.** Chagua jibu linaloonyesha mimea ambayo wanafunzi hupanda kila siku ya wiki.

A. Mikahawa
B. Mipapai
C. Miparachichi
D. Minyanya

---

## SEHEMU B: SARUFI

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 21 hadi 25.**

***(Ni wakati wa alasiri. Mzee Hadi amemtembelea Bibi Mpishe ofisini mwake kusuluhisha mzozo baina yake na maafisa wa haki za watoto.***

**Mzee Hadi** : (*akimpa mkono*) Hujambo Mwanangu?

**Bibi Mpishe** : (*akiupokea mkono*) Sijambo baba. Habari zako na utokako

**Mzee Hadi** : Njema. Nahofia tu za kwako.

**Bibi Mpishe** : ___21___ Nashukuru. (*Anamwashiria kiti aketi*) Asante kwa kukubali mwito wangu. Sitaki kukuweka sana. Naomba niende moja kwa moja kwenye lengo la kukualika hapa. Linahusu bintiyo Viona.

**Mzee Hadi** : Ana nini? Nijuavyo ni kuwa alitoroka nyumbani siku nne zilizopita.

**Bibi Mpishe** : Sababu za kutoroka kwake unazielewa?

**Mzee Hadi** : Hakuna anayejua. Unajua watoto wa siku hizi walivyo wakaidi



CamScanner

**Bibi Mpishe** : (*akionyesha kuudhika*) Mzee Hadi, usiniambie kuwa huna habari yoyote kuhusu mipango ya kumwoza bintiyo akiwa angali mchanga kabla ____23____. Na, ni nani aliyempangia kumkeketa?

**Mzee Hadi** : Mwanangu, unajua mila na desturi zetu. Hiyo ni kawaida kwetu.

**Bibi Mpishe** : Hapo ndipo pana tatizo Mzee Hadi. Ni vyema kutafuta ushauri wa mwanao kabla ya kumuamulia masuala yanayomhusu yeye na haja yanayoathiri afya yake...

**Mzee Hadi** : Hapana! Binti yangu lazima aozwe ili tupate mali lau sivyo atakosa radhi za wazee

**Bibi Mpishe** : (*Kwa mshtuko*) Mzee Hadi, naona hunielewi. Sisi kama watetezi wa haki za watoto tuna jukumu la kuwatetea watoto. Kulingana na sheria, hatma ya Viona ni hii. Atabaki nasi hadi atakapomaliza masomo yake na mwenyewe ataamua kuhusu ndoa yake. Ikiwa hutakubaliana nasi, sitakuwa na jingine ila kukushtaki.

**Mzee Hadi** : Haya basi, kama mtagharamia masomo yake, sina la kusema hata kama mahari ni chakula.

**Bibi Mpishe** : (*anatafakari kwa muda)* Mzee, madeni yako ya mahari ni juu yako. Halafu, mwambie huyo bwana aliyetaka kumuoa Viona, tunamsaka pia. Unaweza kuondoka sasa (*anasimama na kumpa mkono*)

**Mzee Hadi** : (*akiupokea mkono kwa kutetemeka*) Nashukuru kwa mawaidha yako.

**(Wote wanasimama na kuondoka)**

---

**21.** Chagua jibu sahihi kujaza nafasi ya **21** katika kifungu.

A. Kwangu kwema

B. Pangu pema

C. Mwangu mwema.

D. poa

**22.** Kulingana na mazungumzo, Viona alikuwa:

A. Yaya wa mzee

B. Mshukiwa

C. Mkewe mzee Hadi

D. Mwanafunzi

**23.** Chagua nahau ifaayo kukamilisha nafasi ya 23 kwenye kifungu.

A. ya kukata pua aunge wajihi

B. aache mbachao kwa msala upitao

C. ubwabwa hujamtoka shingoni

D. kuona kichefuchefu.

**24.** Mazungumzo haya yamebaini vipengele vifuatavyo vya kusikiliza na kuzungumza ila?

A. Kutumia ishara

B. Kuuliza na kujibu maswali

C. Kuzungumza kwa zamu

D. Kunyamaza kimya

**25.** Mzee Hadi alikuwa amekiuka haki gani ya watoto kwa mujibu wa mazungumzo haya?

A. Haki ya ndoa

B. Haki ya kupata elimu

C. Haki ya kuishi

D. Haki ya kujieleza



CamScanner

**Kifungu kifuatacho kina nafasi ya 26 hadi 35. Umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kujaza nafasi.**

Hakika ____26____mawasiliano kwa njia ya mitandaoni ____27____faida tele kote ulimwenguni. __28__ , tunapaswa kuwa makini kwa lengo la ___29___ uhalifu wa mitandaoni. Watumizi wa mitandao wahakikishe ___30___ kwenye tovuti salama wakati wote. Wafanye tathmini na kuwaweka kwenye mizani wanaosema kuwa ni wandani ___31____ wa mitandaoni kwa kuwa ___32___ . Yasikitisha kuwa idadi kubwa ya watu ___33____ mtandaoni. Serikali inapaswa ___34____ suala hili na kuhakikisha kuwa wahalifu wamefikishwa mahakamani ili ___35____ athibitishe mashtaka yao.

**26.** **A.** .... **B.** ; **C.** : **D.** ,

**27.** **A.** imeleta **B.** zimeleta **C.** yameleta **D.** umeleta

**28.** **A.** Hata hivyo **B.** Kwa hivyo **C.** Ilhali **D.** Kwa sababu

**29.** **A.** kuchochea **B.** kuzuia **C.** kuzuiwa **D.** kuzuilia

**30.** **A.** wanadukua **B.** wanatandawaa **C.** wanasakura **D.** wanatamba

**31.** **A.** zao **B.** kwao **C.** yao **D.** wao

**32.** **A.** mwenye pupa hadiriki kula tamu **B.** usilolijua ni usiku wa giza
**C.** mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani **D.** kinga na kinga ndipo moto uwakapo

**33.** **A.** inalaghaiwa **B.** wanalaghaiwa **C.** zinalaghaiwa **D.**tunalaghaiwa

**34.** **A.** kulivika kilemba cha ukoka **B.** kulivalia njuga
**C.** kulivalia mufti **D.** kulivika kofia

**35.** **A.** kiongozi wa mashtaka **B.** wakili **C.** hakimu **D.** shahidi

---

**Kutoka swali la 36 hadi la 50 chagua jibu sahihi**

**36.** Safu ni kwa mlima kama vile ________ ni kwa sukumawiki.

A. kicha B. chane
C. tita D. mtungo

**37.** Chagua sentensi inayounganisha sentensi zifuatazo ipasavyo.

**Nguo ilikuwa mpya; Nguo haikumpendeza**

A. Mithili ya nguo kuwa mpya haikumpendeza.

B. Nguo ilikuwa mpya angalau haikumpendeza

C. Licha ya nguo kuwa mpya, haikumpendeza.

D. Nguo ilikuwa mpya kwa kuwa ilimpendeza

**38.** Chagua kauli ya kutendewa ya sentensi hii:

**Samba alipiga ngoma akiwa kwa mjomba.**

A. Samba alipigiwa ngoma kwa mjomba

B. Ngoma ilipigiwa kwa mjomba na Samba.

C. Ngoma ilipigiwa. La mjomba na Samba kwake.

D. Mjomba alipigiwa ngoma na Samba kwake.

**39.** Je, nukta pacha hutumiwaje?

A. Kuonyesha ufafanuzi wa maneno ya ziada

B. Kufungia maneno yaliyonukuliwa

C. Kutanguliza maneno katika orodha

D. Kubainisha maneno yaliyotangulizwa.

**40.** Chagua sentensi iliyo katika wakati uliopita hali timilifu.

A. Chakula hakikuwa kikipikwa

B. Kabati imetengenezwa na Seremala.

C. Ng'ombe atakuwa akila nyasi malishoni.

D. Chakula kilikuwa hakijapikwa na mpishi.



CamScanner

**41.** Bainisha neno **lililopigiwa** mstari katika sentensi:

Vikombe **kadhaa** vimeletwa na wanafunzi

A. Kivumishi cha Idadi

B. Kiwakilishi cha Sifa.

C Kivumishi kimilikishi

D. Kivumishi halisi.

**42.** Ni nomino gani iliyo katika ngeli tofauti na nyingine?

A. Maudhui B. Maskani

C. Matagaa D. Maarifa

**43. Chagua wingi wa:**

Kabati lolote utakalonipa nitalipokea.

A. Makabati yoyote watakaonipa nitayapokea.

B. Makabati yoyote mtakayonipa nitayapokea

C. Kabati lolote mtakaonipa nitalipokea.

D. Makabati yoyote watakayonipa nitayapokea

**44.** Panga vifungu vifuatavyo ili viunde sentensi sahihi:

*(i) Kipande cha mbao*

*(ii) huitwa kitata*

*(iii) cha kufungia mkono*

*(iv) Kinachotumiwa na madaktari na wauguzi*

A. i.iii iv ii B. iv iii ii i

C. ii i iv iii D. i. ii iii iv

**45.** Mtu hapaswi kuangazia sana mambo yaliyokwisha kutendeka kwa sababu yanaweza kukufanya usiende mbele. Chagua methali isiyoafikiana na maelezo haya.

A. ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno

B. yaliyopita si ndwele tugange yajayo.

C. maji yakimwagika hayazoleki

D. mavi ya kale hayanuki.

**46.** Chagua usemi taarifa wa:

**" Kikao kitafanyika hapa kesho,"**

Mwalimu aliwaeleza wafanyakazi.

A. Mwalimu aliwaambia wafanyakazi kuwa kikao kingefanyika hapo kesho.

B. Mwalimu aliwaambia wafanyakazi kuwa kikao kingefanyika hapo siku iliyofuata.

C. Mwalimu aliwaambia wafanyakazi kuwa kikao kingefanyika hapa siku iliyofuata.

D. Mwalimu aliwaambia wafanyakazi kuwa kikao kingefanyika hapo siku iliyotangulia.

**47.** Ni sentensi gani iliyotumia kitenzi kishirikishi?

A. Riwaya imesomwa na mwalimu ipasavyo

B. Kosmo amekuwa Marekani.

C. Wanariadha wangali uwanjani.

D. Zainabu alifuzu kwa kuwa anafanya bidii

**48.** Chagua kiambishi kifuatacho kukamilisha sentensi:

**Kipepeo _________mepaa angani.**

A. li B. ki

C. cha D. a

**49.** Chagua ukubwa wa:

**Alitupokea kwa moyo mkunjufu.**

A. lilitupokea kwa joyo kunjufu.

B. Alitupokea kwa jimoyo kunjufu.

C. lilitupokea kwa jimoyo kunjufu.

D. Alitupokea kwa joyo kunjufu.

**50.** Chagua sentensi iliyotumia sitiari.

A. Kanjama alijifunga masombo kazini

B Tina ni duma mbioni.

C. Sonye ni mlafi kama fisi

D. Yuda anajua kikulacho ki nguoni mwako.



CamScanner

# TARGETER WINGS

## KENYA JUNIOR SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT

## GREDI YA TISA - 2026

Wings 001

# KISWAHILI (Insha na Utangulizi wa Fasihi)

**MUDA: Saa 1 dakika 45**

| | |
|---|---|
| Jina la Mtahiniwa ________________ | Nambari ya Mtahiniwa ____________ |
| Jina ya Shule yako________________ | Nambari ya Shule ____________ |
| Sahihi ya mtahiniwa________________ | Tarehe ____________ |

**KJSEA**
**902/2**
**KISWAHILI (Insha na Utangulizi wa Fasihi)**
**Karatasi ya 2**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

1. Andika jina lako na nambari yako ya mtihani kwenye nafasi iliyoachiwa hapo juu.
2. Andika jina na nambari ya shule yako kwenye nafasi uliyoachiwa hapo juu.
3. Tia sahihi kwenye nafasi iliyoachiwa hapo juu.
4. Andika tarehe ya mtihani ipasavyo.
5. Karatasi hii ina sehemu mbili; **A** na **B.**
6. Jibu maswali yote.
7. Andika majibu yote kwa nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki.
8. Majibu yote ni lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| SEHEMU | A | B | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | ZOEZI I Swali:1 | ZOEZI II Swali 2: | Zoezi III Swali 3: | Zoezi IV Swali 4: | Zoezi V Swali 5: |
| Alama ya upeo | 15 | 10 | 10 | 10 | 5 |
| Alama ya Mtahiniwa | | | | | |

**Kijitabu hiki kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**
**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

**FUNGUA KURASA**



CamScanner

**SEHEMU A (Alama 15)**

**ZOEZI I : INSHA**

**Maagizo**

(i) Inapendekezwa uchukue muda wa dakika 40 katika zoezi hili.

(ii) Andika insha yenye maneno kati ya 300 - 350 katika nafasi iliyoachwa.

**Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya..**

.........................................................................Sote tulirudi nyumbani tukiwa na furaha tele.

## SEHEMU B (Alama 35)

## ZOEZI II: FASIHI SIMULIZI (Alama 10)

2. **Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Mtu mmoja alisafiri, naye alikuwa na Ng'ombe jike mmoja. Kabla hajaondoka, alimpeleka ng'ombe wake kwa mtu mmoja katika mji. Na yule mtu alikuwa na Ng'ombe wake dume mmoja. Alipokuwa safarini, Ng'ombe wake akazaa ndama saa sita za mchana.

Safari ikafikia mwisho. Mzee akarudi hadi alikokuwa Ng'ombe wake ili amchukue. Alikuwa amezaa. Alipofika akanena, "nataka Ng'ombe wangu na ndama wake." Yule mzee akamjibu, "nenda zizini ukamchukue Ng'ombe wako. Yule yule uliniachia. Mzee akashangaa na kumwuliza, "Itakuwaje na Ng'ombe wangu alizaa.?

"La, Ng'ombe wangu dume ndiye aliyezaa. Wewe wako alipokuja hakuwa na mtoto na sasa unaweza enda naye," akamjibu. Yule mtu akaenda akisikitika, akafika kwa Abunuwasi. Akamweleza habari iliyompata Abunuwasi akaingia ndani akatwaa nguo za kimaskini akavaa akaenda kwa yule mzee kwa masikitiko sana na kusema, "Mzee nikopeshe shilingi mia tatu, nikamfae baba yangu ambaye amezaa.

Yule mzee akasema, "Usifanye mzaha mimi, kama amezaa mama yako nitakupa." Abunuwasi akasema, "La, hapana bwana, baba yangu ndiye aliyezaa." Yule mzee akanena, "Sijapata kusikia kama mwanamume huzaa.

Abunuwasi akamwambia, "Kama hujasikia leo ndio kwanza." Mzee hakukubali. Abunuwasi akasema, "Kama mwanamume hazai, imekwendaje basi ukanyang'anya Ng'ombe wa huyu kijana? Unasema Ng'ombe wako ndiye aliyezaa naye ni dume. Afadhali ungesema unataka malipo ya uchungaji wako." Yule mtu hakuweza kujibu Abunuwasi tena. Aliwatoa Ng'ombe na ndama na wote akampa mwenyewe.

a) Bainisha kwa kutoa sababu kipera cha hadithi hii. **(alama 2)**

________________________________________

________________________________________

b) Eleza shughuli **mbili** ambazo zinaendelezwa na jamii hii. **(alama 1)**

________________________________________

c) Eleza sifa za Abunuwasi kulingana na hadithi hii **(Alama 2)**

________________________________________

________________________________________

d) Bainisha aina **mbili** za mandhari ambazo zimejitokeza katika hadithi hii. **(alama 2)**

________________________________________

________________________________________



CamScanner

e) Taja mbinu **moja** ya uwasilishaji ambayo fanani angetumia kuwasilisha kauli "usifanye mzaha na mimi, kama amezaa mama yako nitakupa." **( alama 2)**

______________________________________________________________

______________________________________________________________

f) Eleza funzo unalopata kutoka kwa Abunuwasi. **(alama 1)**

______________________________________________________________

**ZOEZI III : NOVELA (Alama 10)**

**3. Soma sehemu ifuatayo ya Novela kisha ujibu maswali.**

Muda wote huo, wazazi wa Chale walikuwa hoi bin taabani kwa wasiwasi. Mzee Jibrili kiti kilikuwa hakimweki tena. Alitembea kutoka sehemu moja ya hospitali hiyo hadi nyingine. Hata wakati mwingine, alitamani kuingia kwenye kambarau za kupandisha watu kutoka ghorofa moja hadi nyingine akidhani ni wadi! Watu waliomwona walidhani ilikuwa mara yake ya kwanza kuwa hospitalini humu. Wengine walidhani alikuwa amepungukiwa na akili. Kunao walioshuku kuwa alikuwa na mgonjwa mahututi, wakamuelewa na kumhurumia. Katika hali hii, Mzee Jibrili aliwaza kuhusu mengi. Aliwaza kuhusu ugonjwa wa mwanawe ambao kwa kweli aliuona kama msiba mkubwa. Aliuona kama ugonjwa uliokuja kumfukarisha zaidi kwa kuwapungusa mifugo wake waliobakia. Ndiyo, huu ulikuwa ugonjwa wa kumfanya hohehahe asiye na mbele wala nyuma.

"Nitatoa wapi ada hiyo ya upasuaji ambayo daktari anadai? Anasema kwamba ada hii ni nafuu. Kwamba angekuwa anaufanyia upasuaji huu katika hospitali ya kibinafsi, ada yenyewe ingekuwa maradufu. Mimi nitazitoa wapi hizo laki anazodai, mkulima na mfugaji mdogo asiye na kingine cha kutegemea? Hata ingekuwa wakati nilipokuwa ninachonga vinyago huko mjini, hela hizo nisingezipata. Ndugu zake chale ndio hao. Mmoja tu ndiye aliyeambulia kibarua juzijuzi. Na usikione kama kibarua chenye kipato.

Ni Kandarasi ambayo itaisha baada ya miezi sita. Huenda waliompa kibarua hicho wasimwite tena. Kunao wengine walio shuleni. Nitawalipia karo ama nitawalipia ada hii ya hospitali? Ama ugonjwa huu unataka nianze kutembea na vibaba viganjani nikiomba mchango ili mwanangu aweze kutoka hospitalini? " Mzee Jabrili alijisemea.

a) Tambua umuhimu wa mandhari katika sehemu hii ya Novela. **( Alama 3)**

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________



CamScanner

b) Eleza mbinu **tatu** za lugha zinazojitokeza katika sehemu hii ya Novela **(Alama 3)**

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

c) Maudhui ni masuala yanayojitokeza katika kazi ya Fasihi. Eleza masuala **mawili** yanayoangaziwa katika sehemu hii ya Novela. **( alama 2)**

______________________________________________

______________________________________________

d) Tambua sifa **mbili** za Jibrili zinazojitokeza katika sehemu hii ya Novela. **(alama 2)**

______________________________________________

______________________________________________

**ZOEZI IV: TAMTHILIA (Alama 10)**

**SEHEMU IV**

**4. Soma sehemu ifuatayo ya tamthilia kisha ujibu maswali**

***(Husda anamrukia Ashua na kumwangusha. Majoka anasimama kando huku akimtazama. Ashua akizabwa makofi Sauti ya Mzee Kenga inasikika mawazoni mwa Majoka.)***

***(Kubali pendekezo letu la kufungwa kwa soko... huoni kuwa hii ni fursa nzuri ya kulipiza kisasi kwa huyo Sudi na kumnasa Ashua? Najua umekuwa ukimmezea mate... akija ofisini... bila shaka, kutatokea patashika na papo hapo, amuru askari wamtie Ashua nguvuni kwa madai ya kuzua vurugu katika ofisi ya Serikali.)***

**Majoka** : (*Kwa ukali huku akielekea kwa Husda na Ashua kuwatenganisha.*) Chopi!

**Chopi** : (*Akifungua mlango*) Yes sir...

**Majoka** : (Anamtoa Husda juu ya Ashua) Mwite Mwango awachukue hawa wanawake wawili. (Ashua na Husda wanashtuka) Sipendi rafu mimi. Sitaki kuambiwa etí, 'ooh! Haki za nani na nani ningewakomesha mimi mwenyewe? (*kwa Ashua na Husda*) Nendeni mpimane nguvu, mpatane msipatane ni shauri yenu. Sina 'time' ya wanawake. (*Mwango na Chopi wanaingia*)

**Majoka** : (*Kwa Mwango na Chopi.*) Wachukueni hawa wawili muwafungie ndani. Msiwachanganye na washukiwa wengine.



CamScanner

**Ashua** : Tafadhali mzee... Wanangu... nanyonyesha... (*Ashua na Husda wanatolewa*)

**Majoka** : Mwango!

**Mwango** : 'Yes sir!'

**Majoka** : Mtoe mama baada ya nusu saa hivi. Mwite dereva wake ampeleke nyumbani. Gari alilokuja nalo utalirejesha baadaye. Mwambie leo nala chapati kwa kuku. Apike yeye mwenyewe.

*(Mwango anaondoka na mlango unafungwa.)*

**Mwisho wa Onyesho.**

a) Eleza umuhimu wa maneno yaliyoandikwa kwenye mabano katika sehemu hii ya tamthilia. (Alama 2)

b) Bainisha aina **mbili** za mandhari zinazojitokeza katika sehemu hii ya tamthilia. (Alama 2)

c) Taja sifa **mbili** za tamthilia ambazo zinajitokeza katika sehemu hii. (Alama 2)

d) Fafanua masuala **mawili** ambayo yameshughulikiwa katika sehemu hii ya tamthilia. (Alama 2)

e) Eleza mbinu **mbili** za lugha zilizotumiwa katika sehemu hii ya tamthilia. (Alama 2)



CamScanner

5. **ZOEZI V: USHAIRI (Alama 5)**

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Njoo tucheze , tucheze kwa heshima
Njoo tucheze, tucheze bila lawama
Njoo tucheze, tucheze kwa salama

Njoo tucheze, tucheze kwa upendo
Njoo tucheze, tucheze bila ya fundo
Njoo tucheze, tucheze kwa mtindo.

Njoo tucheze, tucheze kwa furaha
Njoo tucheze, tucheze bila jeraha
Njoo tucheze, tucheze kwa madaha.

Njoo tucheze, tucheze kwa mafungu
Njoo tucheze, tucheze bila chungu
Njoo tucheze, tucheze kwa udugu.

(a) Kwa kuzingatia idadi ya mishororo, hili ni shairi la aina gani? **Alama 1**

______________________________________________

b) Eleza dhamira ya shairi hili. **Alama 2**

______________________________________________

______________________________________________

c) Mwandishi ametumia mbinu ya urudiaji kwa kiasi kikubwa. Eleza umuhimu wa mbinu hii katika shairi. **Alama 1**

______________________________________________

______________________________________________

d) Je, ni nani anayezungumza katika shairi hili? **Alama 1**

______________________________________________



CamScanner